# MTIHANI WA KUTATHMINI

## KISWAHILI DARASA LA 7 – MEI-

SEHEMU YA KWANZA:

LUGHA

Muda: Saa 1 dakika 40

***Jaza mapengo 1-15 kwa kuchagua jibu liifaalo zaidi***

Mumbi alikuwa___**1**____ kufanya somo____**2**____ alilipenda kutoka utotoni mwake na____**3**____ maana akakataa____**4**____ wa wazazi wake katakata. ____**5**_____wakosane na wavyele____**6**____ hususan babaye kwa kukataa____**7**____ yake kwa muda wa mwaka mmoja .Tulikaa mwaka mmoja bila____**8**____ na babangu kwa kuwa matakwa yalikuwa____**9**____ kupita kiasi. Mumbi alifichua. Kwa kuhofia____**10**_____ ilimbidi Mumbi kujiunga na taasisi ya Jumia kufanya kazi ya____**11**____ hata kama shingo upande. Aliitikia_____**12**____ na chuo hicho ili___**13**_____, eti kageuka____**14**____ mtukutu kwa wazazi wake kwa kuwa amemaliza masomo ya shule ya upili.katika taasisi____**15**____ **,** alisoma sehemu ya kwanza na ya pili ya uhasibu.

**1.** A. anataka B. ametaka C. alitaka D. akitaka

**2.** Ambayo B. ambalo C. ambaye D. ambacho.

**3.** A. ndio B. ndiyo C. ndilo D. ndiye

**4.** A. Mwongozo B. msaada C. mapenzi D. wito

**5.** A. Alitamani B. hakuonelea C. alifurahia D. ilimlazimu

**6.** A. Wake B. yake C. zao . D. lake

**7.** A. Matilaba B. mahitaji C. matakwa D. maoni

**8.** A. kupiga gumzo B. kukanyaga chechele
C. kumpiga mboni D. ulimi mrefu

**9.** A. yakiniumiza B. yakinipa fawaisha C. yakinikera D. yakiniuliza

**10.** A. Msumari moto juu ya donda B. kwenda mrama
C. kupiga mbweu D. maji kuzidi unga

**11.** A. Uhasimu B. uhazili C. uashi D. uhariri

**12.** A. Kujiingiza B. kujiunga C. kujiendeleza D. kujipangia

**13.** A. Asishangiliwe B. asilalamikiwe C. asilaumiwe D. asipendelewe

**14.** A. Kua B. kuua C. kuuwa D. kuwa

**15.** A. hiyo B. hio C. hilo D. hicho

*Kutoka swali la 16-30 jibu kulingana na maagizo uliyopewa*

**16.** Chagua senntensi inayoonyesha maana ya vitate.

A. Bawabu alimpatia bawaba ufunguo wake
B. Mchuuzi Tule alipewa mchuzi mtamu wa nyama
C. Mjuzi yule ana ujusi mwingi wa ujenzi
D. Katika doa ile palikuwa na ndoa

**17.** Chagua sifa tasa katika sentensi zifuatazo.

A. Nywele nyingine hazijachanwa
B. Ondoa ufito huo mrefu hapo
C. Kalamu hii ni ghali mno usiichezee
D. Chai hii ni tamu mno

**18.** Milioni moja, moja elfu na mia moja huandikwaje kwa tarakimi?

A. 1, 001,100
B. 1,100,101
C. 111,001
D. 1,110,100

**19.** Kamilisha methali; Ngombe wa maskini______

A. Ni mnyonge
B. Hakamuliwi asilani
C. Hazai njike
D. Hazai pacha

**20.** Kitendawili tega; wafu wanakokotana

A. Mboga
B. Jahazi na tanga
C. Kufuli
D. Mkufu

**21.** Asile mtoto chakula _______kupashwa moto.

A. Seuze
B. Ila
C. Ijapo
D. Mighairi ya

**22.** Dada na kaka huitana

A. Mpwa
B. Binamu
C. Umbu
D. Kivyele


**23.** Ni nini kinyume cha neno nuna?

A. Furahi
B. Kasirika
C. Nunua
D. Tabasamu

**24.** Sehemu ya nchi kavu iliyozungukwa na maji mengi huitwa

A. Bara
B. Bandari
C. Kilindi
D. Kisiwa

**25.** Umbo hili ni



A. Mche mstatili

B. mstatili

C. mche mraba

D. Hori

**26.** Ni sentensi ipi inayoonyesha KI ya masharti

A. Kijito chenyewe ni kidogo

B. Kichwa chake kimefura kisogoni

C. Alinipata nikidurusu Kiswahili

D. Ukijiona sana huenda hutafanikiwa

**27.** Chagua sentensi iliyotumia viulizi kwa njia bora zaidi

A. Uliniuliza aje jana?

B. Alikuwa mtoto mgani?

C. Atakuja lini?

D. Ulikitumia kisu kigani?

**28.** Chagua nomino isiyoambata miongoni mwa hizi.

A. Batamzinga

B. Kwasababu

C. Garimoshi

D. Njiwamanga

**29.** Neno kasisi liko katika ngeli gani?

A. a-wa

B. i-zi

C. li-ya

D. u-zi

**30.** Kisebeho huliwa wakati gani?

A. Adhuhuri

B. Usiku

C. Mchana

D. Alfajiri

<u>**Soma habari hii kisha ujibu maswali 31- 40**</u>

Watu wengi kote ulimwenguni hawajiamini. Yale wayajuayo ni yale mabaya kuhusu wao wenyewe. Ajabu hii ni kubwa! Ukimwuliza mtu anajua nini ni nadra sana kuwasikia watu wakikiri kuwa wana mengi wayajuayo. Nyakati nyingi ni zile ambazo wakijitazama wataona unyongwe wao.

Dhana hii ndiyo imewafanya mahaluki wengi wenye uwezo wa kufanya makubwa kufa au kuishi katika hali ya ukata mkubwa ajabu. Ningependa kusema kuwa pia wengi wetu wanapenda kuamini kuwa yale mema na makubwa yanaweza kutendwa na wengine na si wao wenyewe. Wivu huwatawala huku wakitamani jasho la wenzao. Inda ikizidi kasi yake

naye ibilisi hupata pa kukaa akawapa mijikono na simikono ya kutenda bali mirefu ya kuasi sheria.

Wapo wachache ambao hali yao sasa huwa daraja kuu mno ya kuwarusha upande wa pili wa maisha. Hawa ni wale hutambua wazi kuwa Rabi msta katika taamuli uwezo na mapenzi alimwumba mja razini mwenye uwezo wa kipekee. Ugunduzi huu huwapatia ari ya kutenda kila walitendalo. Hawa ni watu ambao wamefaulu zaidi maishani mwao.

Baadhi yetu tunapenda kusema fulani amebarikiwa;mbona sio wewe? Wengine hujitilia balaa kwa kutenda maovu ambayo hayalipi chochote na hapo Manani ana njia yake ya kujilipizia. Huwanyima Baraka zake.

Twafaa kusikia sauti ndani yetu ambayo hutuambia tunaweza!!!

**31.** Watu wengi
- A. Unyonge wao huchukua sehemu kuu ya mawazo yao
- B. Wanajielewa vyema
- C. Hawajielewi wala hawana mabaya
- D. Matendo yao mema huwa wazi

**32.** Kulingana na makala haya
- A. Watu wengi wanajipenda sana
- B. Watu wengi hawajui chochocte kabisa
- C. Japo watu wengi wanajua mengi hawaamini hivyo
- D. Wanajua kila jambo

**33.** Mbona watu wengi hufa katika hali ya umaskini?
- A. Hawana taaluma yoyote
- B. Hawajiamini kutenda mambo kadri ya uwezo wao
- C. Ni wanyonge wa hali na mali
- D. Hawana mwongozo dhabiti

**34.** Neno **<u>nadra</u>** limetumiwa kumaanisha
- A. Ni vigumu sana
- B. Rahisi
- C. Ni kawaida
- D. Halikadhalika

**35.** Ni kweli kusema
- A. Watu wengi hujua yale mabaya yanayowahusu
- B. Watu wengi hujua yale mazuri yanayowahusu
- C. Watu wengi hawajali yanayowahusu
- D. Watu wengi si wabaya

**36.** Twaangaziwa watu wengi huiba kwa sababu ya
- A. Wivu wa fanaka za wenzao
- B. Kukosa dini na kumfuata ibilisi
- C. Kukosa maarifa ya kutenda mambo
- D. Kuwa na mikono mirefu zaidi

**37.** Wale ambao hufaulu

A. Huwa na nguvu za kipekee za ajabu
B. Ni wajanja katika matendo na mawazo
C. Huandamana na njia fisadi maishani
D. Huelewa mawazo ya muumba wao kwao

**38.** Ni kweli kusema

A. Kila mtu hana uwezo wa kutenda mambo yote
B. Maulana anawapenda wengi wala sio wote
C. Mawazo yetu hayatuambii ukweli wetu
D. Maovu yanaweza kutulhetea balaa kuu

**39.** Ni semi ipi inayomaanisha kutia nuksi au bahati mbaya?

A. Angukiwa na nyota ya jaha
B. Tia ukuba
C. Tia mrija
D. Kanyaga chechele

**40.** Kulingana na makala haya twaweza kusema

A. Ni bora kujiona wenye uwezo kuliko wanyonge
B. Tujipeleleze ili tupate kujielewa unyonge wetu
C. Sote tulazimu Mungu atupe Baraka
D. Hatuna uwezo wa kutenda mema yoyote

**Soma habari hii kisha ujibu maswali 41-50**

Tuliachana vizuri na Emma na tukapeana mkono wa buriani kwa huzuni kwani mtoto huyu alizaliwa akazalika na alinifaa tangu nilipokuwa shule ya msingi darasa la nane. Huu ndio wakati uliokuwa mgumu zaidi katika aushi yangu . Ulikuwa umenifanya kushuku kuwa Maulana alikuwa ameniachia ibilisi anitese.

Mkururo wa baa, balaa na beluwa viliniganda kama kupe na mkia wa bakari. Sisi kwetu tulikuwa ndugu watatu wa kiume. Nina hakubahatika kupata binti. Basi mwaka huo kaka yangu , kifungua mimba alikuwa akinifaa katika mawazo, akiniongoza kuwa na hulka bulibuli na tasfida ya ajabu. Alizuru mava kwa njia ya ajali ya maji kilindini. Hapa nililia kwa shake, machozi makuu yakinipukutika, lakini sikuwa na langu. Wakale walinena yuende aendaye mwenda kweli hana marejeo na kiendacho mava hakina marejeo.

Nilikuwa nafuu kidogo kwani nilikuwa na kaka wa kukaa naye. Aidha, tulikuwa wengi kwa hivyo bashasha zilirudi. Siku korija baadaye abu, nina na kakangu waliabiri gari kwa dharura ya kumwona bibi ambaye alikuwa hoi. Waliniacha maskini peke yangu ati wangerudi alasiri ile. Hili lilikuwa jinamizi. Huo ndio ulikuwa wakati wangu wa mwisho

kuwapiga mboni. Yaliyofuata baadaye ni halaiki ya watu mmoja mmoja wakileta tanzia zao na makiwa.

Basi hapo nilijua sina langu. Wote walikuwa wameniasi katika ulimwengu huu wenye shida na malimwengu yake. Sikuwa na wakukulia wala wa kunikimu mpaka Emma aliponijia.

Ingawa sasa nilikuwa nimebahatika mithili ya tasa aliyepata mwana wa kike, sikuwa naamini naenda kuishi bara jingine na kuwa pengine nisingepata fursa ya kumkimu binti mtu huyu katika uzee wake.

**41.** Emma alikuwa

A. Nyanya yake mwandishi
B. Mamaye wa kupanga
C. Shangaziye
D. Rafiki tangu utotoni

**42.** Ni sentensi ipi inayoelezea hali ya awali ya mwandishi?

A. Aliishi kwa furaha huku akiongozwa nyuma
B. Aliishi peke yake aushi yake yote
C. Hakupata mafunzo ya adabu
D. Aliachana na Emma baadaye

**43.** Kwa nini mwandishi anamwita Emma "mtoto"?

A. Alikuwa mwenye umri mkubwa kuliko Emma
B. Umbo lake lilipendeza kama la mwana mchanga
C. Alimdharau kwani alikuwa mseja
D. Lilikua jina lake la pili

**44.** Aila yake mwandishi ilikuwa ya watu wangapi?

A. Sita
B. Watatu
C. Wawili
D. Watano

**45.** Habari za tanzia ni habari za

A. Buriani
B. Matangazo ya habari
C. Kifo
D. Hongera na mafanikio

**46.** Kakaye kifungua mimba alifariki

A. Kwa kuzama majini
B. Ajali ya barabarani
C. Alipigwa risasi
D. Aliugua akafa

**47.** Balaa iliyofuata kifo cha kakaye ilitokea baada ya muda gani?

A. Siku ishirini
B. Mwezi mmoja
C. Robo ya mwaka
D. Mwongo mmoja

**48.**“basi hapo nilijua sina langu” yaani

A. Alibaki mrithi wa mali yote
B. Alibaki na nyanyaye pekeyake
C. Alibaki hohehahe hana mbele wala nyuma
D. Aliachwa ajitawale mwemyewe

**49.**Hofu kubwa ya mwandishi ni kuwa

A. Nduguze waliaga dunia akiwa mchanga
B. Alilelewa na mtu mwingine
C. Alitaka nafasi ya kumtendea wema Emma ambayo haikuwa dhahiri
D. Hakutaka kusafiri nchi za mbali ambako alilazimika kwenda

**50.**Twaweza kukubaliana na methali ipi kati ya hizi

A. Adui mpende
B. Mwenda tezi na omo marejeo ni ngamani
C. Akuufaaye kwa dhiki ndiye rafiki
D. Hakuna msiba usiokuwa na mwenziwe